# ORODHA YA KANUNI ZA

# Mafanikio

Said Maumba
Mwanzilishi wa MAUMBA BLOG



# KUHUSU SAID MAUMBA

**Bw. Maumba Said B,** ni mzaliwa wa Jijini Dar es salaam. Ni kijana mwenye kipaji cha uandishi, ni msanii wa mashairi ya kuzungumza (*Spoken poetry artist*), Mzungumzaji wa hadhira (*Public speaker*), Muigizaji lakini pia ni mwandishi katika blogu yake iitwayo **MAUMBA BLOG**.

Wasiliana Nae Kwa E-Mail:-

Maumba225@gmail.com

Au tembelea blog yake

https://www.saidmaumba.co.tz

## 06. SOMA. TAFUTA UJUZI NA MAARIFA

Kusoma hakuishii shuleni. Na kama kuna shule basi, maisha ndiyo shule kubwa kuzidi hata hiko chuo kikuu.

Yani iko hivi, hata ukipata Phd. Bado tuu lazima uje kwenye darasa hili, yani maisha. Hivyo basi, naamini kusoma ni moja kati ya shughuli za muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku.

Jifunze ujuzi kwa kuhudhuria kozi mbalimbali. Soma vitabu na ujiongezee maarifa mapya na yanaolipa yatakayozidi kukusaidia kuishi maisha bora na kukuletea mafanikio zaidi.

Nasema hivi, kila siku hakikisha unasoma sana, kwa lengo la kutafuta ujuzi (*Na sio vyeti tu. Mana naamini kwamba, vyeti huwa vinakupa nafasi ya kuaminika na watu. Ila vyeti havifanyi kazi. Ni ujuzi wako ndio haswa unaoleta matokeo na thamani*)

Nimesema SOMA. Lakini, ***kusoma sio lazima vitabu bali hata kwa kutembelea tovuti (Websites) na blogu mbalimbali. Humo unaweza kujifunza SKILLS nyingi sana bila malipo. Binafsi ujanja na ujuzi mwingi sana nilio nao ni sehemu ya mafunzo na vitu nilivyosoma kutoka mtandaoni.***

*Basi kama hutojali Karibu sana kwenye blog yangu.* ***KARIBU MAUMBA BLOG***. Lakini pia, unaweza kusoma hata kupitia aina ya videos unazozifuatilia *YouTube* na mitandao mingine ya kozi za mafunzo (*Online Courses*) mathalan, *Udemy, Alison Courses na kadhalika*.

## 07. JIFUNZE SANA NA UIFAHAMU SANA TEKNOLOJIA.

Moja kwa moja basi hapa ningesema, jitahidi sana uwe na Digital skills.

Yani kwa namna dunia yetu hii inavyoenda, basi baadae (*Na hata sasa*) ***watu wenye ujuzi wa teknolojia na masuala ya kidijitali watakuwa na uwezo mkubwa wa kuziona na kuzitumia fursa kujijengea mafanikio yao.***

Ni ulimwengu wa teknolojia na taarifa, ndio maana nakwambia jifunze sana na uifahamu teknolojia halafu relax, najua tu lazima itakusaidia sana sasa na hata baadae.

Na kama ukikusudia kujifunza kwelikweli basi jitahidi sana kuhudhuria madarasa na kozi mbalimbali. Sina shaka kwamba ujuzi wako utakulipa.

Utakulipaje?

Utakulipa kwa kukusaidia wewe mwenyewe kuongeza ushindani sokoni. Lakini pia utakusaidia kwenye biashara yako, kama hauna biashara basi pengine kwenye ajira yako. Ila kikubwa hakikisha

unajifunza na kuifahamu sana teknolojia haswaa kuwa na hizo digital skills.

## 08. TENGENEZA TIMU YAKO YA WATU SAHIHI.

***"You'll never walk alone!"*** hivyo ndivyo mashabiki wa Liverpool wananavyokuambia. Basi ni kweli ***hata kwenye mafanikio, unaambiwa kuwa "You'll never win alone!" ni lazima uwe na watu.***

Ni lazima uwe na timu ya watu wako mtakaoshirikiana.

Kwani haujawahi kusikia msemo unaosema, ***"Teamwork makes dream work"***, kama haujawahi kuusikia basi ndo ushausikia hapa. Na kitu kikubwa ninachomaanisha ni kwamba, kila siku hakikisha na ujitahidi sana kwenye kutafuta watu sahihi na kisha kuunda nao timu mtakayoshirikiana kwenye mipango na ndoto zenu.

Watu wengi hapa huwa wanafeli! Ila kiukweli team yako ndio marafiki zako.

Na kama ukiniuliza, “Kwanini tunao marafiki?” basi hii ni moja ya sababu kwanini haswaa tunao marafiki.

Okei, point yangu ni kwamba, awe ni rafiki yako mliyezoeana sana au mtu tu mliyekutana hivi karibuni lakini hakikisha unakuwa na timu ya watu sahihi. Na nikisema timu namaanisha kila mmoja katika timu ujue mnaweza kusaidiana na kuchangiana vipi, yani katika kipi na lipi kwenye kutimiza malengo, pamoja na ndoto zenu.

***Without a team of right people, huwezi kutoboa ndugu yangu.*** If you think naweza kuwa kwenye team yako, usisite kuwasiliana na mimi kwa KUBOFYA email hii hapa, maumba225@gmail.com

## 09. TEKELEZA KILA UNACHOKISOMA.

Watu wengi watakuambia ukitaka kufanikiwa basi soma sana vitabu. Ni kweli hata mimi niliwahi kuambiwa hivyo, na ninasoma sana vitabu!

Malalamiko makubwa huwa ***"Mbona nasoma sana vitabu, tena vingi lakini havinisaidii na sioni mafanikio?"***.

Ukweli ni kwamba... ***sio tuu kusoma vitabu bali siri ipo kwenye kufanyia kazi na kutekeleza mafunzo na masomo uliyoweza kujifunza kutoka kwenye vitabu husika.***

Kwahiyo hata hapa ndani ya kitabu hiki, utasoma na kujifunza mafunzo mengi sana. Lakini ***kufanikiwa kwako kutategemea na kiwango na bidii ya utekelezaji wa mafunzo uliyojifunza***.

Naomba sasa kwa masikitiko makubwa nikwambie hivi, *"Hatufaniikiwi kwa kusoma vitabu, bali*

*tunafanikiwa kwa kutekeleza kile kitu tulichoweza kujifunza kutoka kwenye hivyo vitabu tulivyovisoma"*

## 10. USIKATE TAMAA!

Naomba irudiwe hiyo, yani sio kurudia kuisoma hii point. Hapana! Maana yangu ni irudiwe kwa mara nyingine tena kufanya hicho kitu ulichokuwa unakifanya kabla hujaamua kukata tamaa na kukiacha kabisa.

Unajua ***kwenye maisha kuna baadhi ya vitu hatufanikiwi kwa kuvifanya mara moja tu! Bali vinahitaji tuweze kuvirudia mara kwa mara.*** Na hapo ndipo ilipo siri ya mafanikio makubwa ya watu wengi sana.

Nasema hivi ukweli utabaki kuwa ukweli. Ukweli ni kwamba, *watu waliofanikiwa na watakaoendelea kufanikiwa ni wale ambao kwao wao kushindwa baada ya kujaribu ndiyo passion yao. Na badala ya kuwa kikomo cha kuwakomesha, ndiyo kwanza*

*huona ni fursa mpya ya kuanza tena na kurudia kile walichofeli mara ya kwanza. Isipokuwa sasa, muda huu hujitahidi kutoyarudia yale makosa ambayo walijifunza kutokana na kufeli kwao mara ya mwisho.*

***Wao hawafahamu kabisa, na akilini mwao wameshafuta kitu kinachoitwa, "Kukata Tamaa". Wanachoamini na wanachofurahia wao ni, "Kujaribu tena! Yani tena na tena mpaka kufanikiwa".***

Hao ndio watu ambao naandika hapa nikikushauri uweze kuwa mmoja wao. Achana na huko unakotaka kwenda, acha kujiunga na watu wenye kukata tamaa. Na kama kuna watu wanaokukatisha tamaa basi Jifunze kukabiliana na watu wanaokukatisha tamaa mapema sana ili usipoteze mafanikio yako.